majira

8 HABARI

Ijumaa Julai 6, 2012

# UCHUMI & BIASHARA u&b

Business Leaders Perception Report 6 July 2012 Majira Page 8

## Wafanyabiashara wataka uwazi katika kodi

Na Hyasinta Timothy

ASILIMIA kubwa ya wafanyabiashara wa utalii nchini wapo tayari kulipa kodi kama serikali itaweka utaratibu na mfumo wa wazi utakaoonesha jinsi fedha hizo zinavyotumika kwa ajili ya manufaa ya taifa nzima.

Hayo yamo katika uchambuzi wa ripoti ya nne ya kila mwaka ya mtazamo wa viongozi wa biashara nchini Tanzania ambayo inatoa muhtasari wa mitazamo yao kuhusu mazingira wezeshi na nafasi ya serikali katika kuhakikisha biashara inafanywa kwa urahisi.

Ripoti hiyo imeratibiwa na BEST-AC, taasisi ambayo husaidia Jumuiya za Sekta Binafsi (PSOs) kushiriki katika mazungumzo kati ya sekta binafsi na ya umma kwa lengo la kushawishi mabadiliko kwenye sera za umma za kuboresha mazingira ya biashara Tanzania. Mchambuzi wa ripoti hiyo ni Bw.David Irwin, ambaye ni mtaalamu wa masuala ya uchumi.

Mchambuzi wa ripoti hiyo Bw.David Irwin alisema kwenye ripoti hiyo biashara ya utalii inatambua kuwa wakati wote kuna umuhimu wa kulipa kodi. Hata hivyo wahojiwa wengi kwenye utafiti huu wanaona kuwa kupungua kwa mzigo wa mlolongo wa urasimu ungeisaidia sketa hiyo vizuri zaidi.

Alisema pia kuwa wafanyabiashara walipendekeza kuwepo kwa mfumo mmoja wa kusaidia serikali kupata mapato kutoka kwenye sekta hii na wakati huohuo kuweka mfumo madhubuti ambao utapunguza gharama ya kufanya biashara na kuwapatia wafanyakazi muda wa kujihusisha na kazi zinazohusiana na biashara yao, kama vile kutafuta masoko, kutoa mafunzo na kujenga uhusiano na wateja.

Bw. Irwin anawanukuu wafanyabiashara ya utalii wakielezea kuwa urasimu usio wa lazima unaleta matatizo kwenye biashara, na kusisitiza kuwa wafanyabiashara wanatambua kuwa serikali inahitaji kukusanya mapato.

Ripoti hiyo ya mtazamo wa wafanyabiashara iliandaliwa ili kutoa vidokezo vya vipaumbele vya kufanyiwa kazi kwa lengo la kuboresha mazingira ya kufanya biashara Tanzania.

Utafiti wa mitazamo ya wadau wa biashara na mazingira ya uwekezaji Tanzania uliofanyika 2011, ulibainisha maoni ya wadau hao kuhusu mazingira ya uwekezaji Tanzania.